



**CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA ELIMU
DAR ES SALAAM**



**MWONGOZO WA MAVAZI KWA WANAJUMUIYA NA WAGENI WA
CHUO**

APRILI 2018

Yaliyomo

1.0 Utangulizi.....	1
2.0 Hali ya Uvaaji Ilivyo kwa Sasa.....	2
3.0 Mwongozo wa Mavazi kwa Watumishi, Wanafunzi na Wageni.....	3
3.1 Mavazi na Muonekano Usiofaa kwa Watumishi	4
3.1.1 Watumishi wa Kike.....	4
3.1.2 Watumishi wa Kiume.....	5
3.2 Mavazi na Muonekano Usiofaa kwa Wanafunzi	5
3.2.1 Wanafunzi wa Kike.....	5
3.2.2 Wanafunzi wa Kiume.....	6
3.3 Mavazi na Muonekano Usiofaa kwa Wageni	6
3.3.1 Wageni wa Kike.....	6
3.3.2 Wageni wa Kiume.....	7
3.4 Mavazi Yasiyotarajiwa kwa Watumishi, Wanafunzi na Wageni.....	7
4.0 Utekelezaji wa Mwongozo wa Mavazi Yanayozingatia Maadili kwa Watumishi, Wanafunzi na Wageni	7
5.0 Hitimisho.....	8
Marejeo	9
OFISI YA RAIS	13
WARAKA WA UTUMISHI WA UMMA NA 3 WA MWAKA 2007 KUHUSU MAVAZI KWA WATUMISHI WA UMMA.....	13
George D. Yambesi.....	16
KATIBU MKUU	16

1.0 Utangulizi

Uvaaji wa mavazi yanayozingatia maadili siyo jambo geni kwa watumishi wa umma na jamii kwa ujumla. Mwongozo wa uvaaji wa kuzingatia maadili kwa watumishi wa Umma ulitolewa na Serikali kwa mara ya kwanza kupitia Waraka Na. 1 wa mwaka 1971. Madhumuni ya Waraka huo ilikuwa ni kuimarisha heshima ya Taifa kwa kuhakikisha kuwa watumishi wa Serikali wanavaa mavazi ya heshima wanapowahudumia wananchi. Waraka huo uliainisha baadhi ya mifano ya mavazi ambayo yalionekana hayafai na yale yanayofaa kwa wanawake na wanaume, utengenezaji wa nywele unaofaa na usiofaa na vipodozi visivyokubalika.

Tarehe 12 Septemba, 2007 Serikali ilitoa Waraka Na. 3 kuhusu Mavazi kwa Watumishi wa Umma wenye madhumuni yaliyoainishwa hapo juu ikiwa na lengo la kuuboresha Mwongozo wa Waraka Na. 1 wa mwaka 1971. Aidha Waraka huu ulifafanua kuwa katika Utumishi wa Umma, mavazi ya heshima kwa watumishi wa Umma ni yale ambayo yanazingatia mila na desturi za Taifa letu ambayo yanapovaliwa hayaonyeshi sehemu ya maungo ya mwili ambayo hayakuzoeleka kuachwa wazi, hayabani na ambayo hayana michoro au maandishi ya kudhalilisha wengine au yanayoonesha ushabiki wa kitu fulani.

Tangu kutolewa kwa miongozo hiyo kupitia Nyaraka za Serikali, waajiri wamekuwa wakiwaelimisha watumishi kuhusu mavazi yasiyokubalika na kusimamia kikamilifu suala la mavazi kwa Watumishi wa Umma.

Mwishoni mwa mwezi Februari 2018, Chuo kilipokea taarifa toka Serikalini kuhusu uvaaji wa wanafunzi usiozingatia maadili. Katika hatua ya kutekeleza maelekezo ya Serikali, Chuo kiliandaa taarifa kuhusu uvaaji wa wanafunzi na kuiwasilisha Serikalini kupitia Wizara ya Elimu na Teknolojia. Aidha, pamoja na kuwasilisha taarifa hiyo Chuo kiliandaa mabango yanayoonesha uvaaji usiozingatia maadili kama hatua ya kuzuia uvaaji usiofaa kwa watumishi, wanafunzi na wageni.

Kwa kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam ni miongoni mwa taasisi za Umma kinawajibika kuzingatia miongozo inayohusu uvaaji wa mavazi yanayozingatia maadili kama ilivyoainishwa na Serikali kupitia Nyaraka zilizotajwa hapo juu. Hivyo, Chuo kinawajibika kuhakikisha kuwa watumishi wake, wanafunzi na wageni wanazingatia uvaaji unaozingatia maadili wanapokuwa katika mazingira ya Chuo. Aidha, kwa kuzingatia Maadili ya Utumishi wa Umma, Mtumishi wa Chuo anawajibika kuzingatia uvaaji unaozingatia maadili hata akiwa nje ya mazingira ya Chuo ili kulinda hadhi ya

Utumishi wa Umma. Wanafunzi pia wanawajibika kuvaa mavazi yanayozingatia maadili wanapokuwa nje ya mazingira ya Chuo ili kulinda hadhi ya Chuo kwa kuwa wao ni mfano bora wa Chuo na wanaandaliwa kuwa watumishi wa umma hapo baadaye.

Mwongozo huu unakusudia kuwaelekeza wanajumuiya wa Chuo kuzingatia uvaaji unaofuata mila na desturi za Taifa ikiwa ni utekelezaji wa maagizo ya Serikali yanayohusu uvaaji wa kimaadili.

2.0 Hali ya Uvaaji Ilivyo kwa Sasa

Kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia na maendeleo mbalimbali ulimwenguni, kumekuwa na wimbi la ongezeko la wananchi kuiga mifumo ya maisha ya maeneo mbalimbali ya dunia hususani Ulaya na Amerika. Mifumo hii ya maisha inajumuisha mavazi ambayo yapo katika mitindo mbalimbali. Hali hii imepelekea watu wazima kwa wadogo kubadili mienendo yao ya kimaisha katika nyanja mbalimbali kama vile vyakula, lugha, mahusiano na mavazi na kusahau kabisa mienendo ya maisha inayoendana na maadili yanayozingatia mila na desturi za Taifa letu. Aidha, hali hii imesababisha madhara kwa jamii kama vile kuongezeka maradhi yasiyo ya kuambukiza, migogoro ya kifamilia, matukio ya kihalifu, uvaaji unaokiuka maadili n.k.

Kama ilivyo kwa baadhi ya taasisi nyingine za Umma, watumishi na wanafunzi wachache huvaa sare katika mazingira maalumu. Watumishi hawa ni watumishi katika Zahanati ya Chuo, Polisi Wasaidizi na watumishi wa Maabara, ambao huvaa sare wanapokuwa kwenye majukumu yao. Wanafunzi wanaovaa sare ni wa shule za mazoezi Chang'ombe, yaani Awali, Msingi na Sekondari na wanachuo wanaosomea masomo ya sayansi na wanavaa sare wanapokuwa kwenye mafunzo kwa vitendo. Watumishi na wanafunzi wengine hawalazimiki kuvaa sare na hivyo kuwa huru kuvaa mavazi watakavyo. Hali hii imechochea watumishi na wanafunzi kuvaa mavazi yasiyofaa kwa utumishi wa Umma. Hata hivyo, kwa kuwa lengo la Chuo ni kuwaandaa wanafunzi kuwa wanajamii wanaofuata maadili mema, Chuo kimekuwa kikiwasisitiza kuvaa mavazi yanayoendana na mila na desturi za Taifa ikiwa ni pamoja na kufundisha maadili ya ualimu ambayo yanajumuisha na mavazi ya mwalimu. Masomo yanayogusia maadili ya wanafunzi ikiwa ni pamoja na mavazi ni CT 100 (*Introduction to Teaching*), CT 106/107 (*Language Teaching Methods*), CT 108 (*Science Teaching Methods*) na EF 303 (*Ethics and*

Professionalism in Education). Aidha kumekuwepo na kampeni ya kuhamasisha uvaaji bora kwa wanafunzi iitwayo “Decent wearing”.

3.0 Mwongozo wa Mavazi kwa Watumishi, Wanafunzi na Wageni

Sehemu hii imeainisha aina ya mavazi yasiyofaa kwa watumishi, wanafunzi na wageni kwa kuzingatia jinsia za makundi haya matatu.

Ili kubainisha aina za mavazi yasiyofaa kwa watumishi na wanafunzi, mwongozo huu unaainisha aina ya mavazi yasiyofaa kuvaliwa ili watumishi wawe na utambuzi wa mavazi haya usio na shaka.

Lengo la mwongozo huu ni kuwa na watumishi na wanafunzi nadhifu wakati wote na kujenga hali ya kujiamini kwa watumishi wanapohudumia wanafunzi na wageni toka nje ya Chuo. Hali hii pia hujenga imani kwa wanafunzi na wageni pale wanapohudumiwa na watumishi wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam.

Chuo kinatambua kuwa uvaaji wa watumishi na wanafunzi una umuhimu mkubwa kwa kuwa unaakisi hadhi ya Chuo, hivyo watumishi wanahimizwa kuvaa mavazi yanayozingatia maadili ili kutoathiri hadhi ya Chuo na watumishi wenyewe kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Pamoja na kuwa Chuo kinazingatia uwepo wa mila, desturi na dini mbalimbali, inasisitizwa kuwa mavazi yatakayoendana na mila, desturi au dini yanayokiuka maadili ya Utumishi wa Umma hayatavamiliwa. Hata hivyo, kwa kuwa Chuo kinatambua uwepo wa watumishi na wanafunzi wenye aina tofauti za ulemavu, kinawapa watumishi au wanafunzi hawa uhuru wa kuvaa mavazi ambayo hayatakuwa kikwazo kutokana na hali zao za ulemavu.

Mwongozo huu unawaelekeza viongozi wa ngazi mbalimbali na watumishi wa Chuo kuzingatia uvaaji unaozingatia maadili ya Utumishi wa Umma. Mwongozo huu haujataja aina zote za mavazi yanayofaa na yasiyofaa kwa watumishi wa Chuo, hivyo watumishi wanaaswa kutumia ufahamu wao kutambua mavazi yasiyofaa kuvaliwa na hayakuainishwa kwenye mwongozo huu.

Chuo kinatambua kuwa kuna watumishi ambao kutokana na kazi zao wanavaa sare. Watumishi hawa wanalazimika kufuata mwongozo huu kwa kuvalia sare hizo kulingana na mwongozo wa sare za taaluma zao (*Professional dress code*) na maagizo ya wakuu wa maeneo yao juu ya uvaaji wa sare hizo.

Watumishi wote wanatakiwa kuvalia vitambulisho vyao vya kazi wakati wote wawapo katika maeneo ya Chuo au wanapokuwa nje ya eneo la Chuo kikazi kwa namna yoyote ile. Hii itarahisisha utambuzi wa watumishi na wasio watumishi. Pamoja na kuleta unadhifu

kwa watumishi, uvaaji wa vitambulisho vya kazi unasaidia kuimarisha usalama kwa watumishi, wanafunzi na Chuo kwa ujumla.

Watumishi, wanafunzi na wageni wa Chuo wanatakiwa kufuata mwongozo huu. Endapo mtumishi au mwanafunzi atakiuka maelekezo ya mwongozo huu atambue kuwa itakuwa ni utovu wa nidhamu na hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake. Aidha, endapo aliyekiuka maelekezo ya mwongozo huu ni mgeni, atazuiwa kuingia maeneo ya Chuo na kunyimwa huduma muhimu za kiofisi.

Viongozi wa ngazi zote wanawajibika kuhakikisha kuwa watumishi au wanafunzi walio chini ya mamlaka yao wanazingatia maelekezo ya mwongozo huu juu ya uvaaji wa mavazi yanayoendana na maadili wakati wote wawapo katika maeneo yao ya kazi. Kiongozi atakayeshindwa kusimamia mwongozo huu katika eneo lake la mamlaka atawajibika kwa kushindwa kutimiza wajibu wake.

3.1 Mavazi na Muonekano Usiofaa kwa Watumishi

3.1.1 Watumishi wa Kike

(i) Mavazi yasiyofaa:

- a) Nguo zinazobana;
- b) Nguo fupi ambazo zinaacha magoti wazi;
- c) Nguo ambazo zinaacha sehemu ya mwili wazi kama vile kitovu na kifua;
- d) Nguo ambazo zina picha, michoro, na maandishi ambayo hayaendani na shughuli za serikali;
- e) Kaptura aina yoyote ile kama vile pedo na pensi;
- f) Nguo zinazoonyesha maungo ya mwili (*Transparent clothes*);
- g) Suruali za '*Jeans*';
- h) Suruali yoyote iliyoachwa bila ya kupindwa;
- i) Fulana – "*T-Shirts*" (Hizi zivaliwe tu wakati wa shughuli maalumu inayotambulika).
- j) Nguo ambazo ni za kazi maalumu – michezo, kazi za nje au burudani. Hizi zivaliwe mahususi wakati wa utekelezaji wa shughuli hizo;
- k) Nguo yenye maandishi ya chama chochote cha siasa au ushabiki wa kitu fulani;
- l) Sketi zenye mpasuo mkubwa;
- m) Niqab (Mtandio unaofunika sura na kuacha macho tu);
- n) Baibui;
- o) Nguo yoyote isiyoendana na maadili ya Taifa;

(ii) Nywele zisizofaa:

- a) Nywele chafu na ambazo hazikutengenezwa vizuri

(iii) Viatu visivyofaa:

- a) Kandambili;
- b) Viatu vya michezo (isipokuwa wakati wa shughuli maalumu za michezo)

3.1.2 Watumishi wa Kiume

(i) Mavazi yasiyofaa:

- a) Nguo ambazo ni za kazi maalumu kama vile michezo haziruhusiwi kuvaliwa wakati ambao si wa kazi hiyo. (Hizi zinatakiwa kuvaliwa wakati wa shughuli hiyo tu);
- b) Nguo ambazo zina michoro, maandishi na picha ambazo haziendani na shughuli za serikali;
- c) Nguo zinazobana;
- d) Kaptura ya aina yoyote;
- e) Suruali yoyote inayoachwa bila ya kupindwa;
- f) Suruali za 'Jeans' na fulana 'T-Shirts' (Hizi zivaliwe tu wakati wa shughuli maalumu inayotambulika);
- g) Kikoi au msuli;
- h) Nguo zenye maandishi ya chama chochote cha siasa na yenye kuonyesha ushabiki wa kitu fulani au kuwa na lugha chafu;
- i) Suruali inayoonyesha sehemu ya makalio (*Mlegezo*);
- j) Uvaaji wa hereni;
- k) Shati lisilofungwa vifungo na vesti;
- l) Kofia;
- m) Kanzu;
- n) Nguo yoyote isiyoendana na maadili ya Taifa.

(ii) Nywele zisizofaa:

- a) Nywele chafu;
- b) Nywele ambazo hazikutengenezwa vizuri;
- c) Nywele zilizosukwa mtindo wa aina yoyote ile;
- d) Nywele zilizonyolewa kwa mtindo usio wa maadili mfano; *kiduku, denge* n.k.;
- e) Ndevu zisizotunzwa vizuri;

(iii) Viatu visivyofaa:

- a) Kandambili;
- b) Makubadhi;
- c) Viatu vya michezo (labda wakati wa shughuli maalum ya michezo).

Rejea *Kiambatisho Na. 1* (Kielelezo cha mavazi kwa watumishi wa umma kwa mujibu wa Waraka wa Utumishi wa Umma Na. 3 wa Mwaka 2007)

3.2 Mavazi na Muonekano Usiofaa kwa Wanafunzi

3.2.1 Wanafunzi wa Kike

(i) Mavazi yasiyofaa:

- a) Nguo zinazobana;
- b) Nguo fupi ambazo zinaacha magoti wazi;
- c) Nguo ambazo zinaacha sehemu ya mwili wazi kama vile kitovu na kifua;

- d) Nguo ambazo zina picha, michoro, na maandishi ambayo hayaendani na shughuli za serikali;
- e) Kaptura aina yoyote ile kama vile pedo na pensi;
- f) Nguo zinazoonyesha maungo ya mwili (*Transparent clothes*);
- g) Suruali za '*Jeans*' zinazobana na kuonesha maungo na zilizochanwa;
- h) Suruali yoyote iliyoachwa bila ya kupindwa;
- i) Nguo yenye maandishi ya chama chochote cha siasa au ushabiki wa kitu fulani;
- j) Sketi zenye mpasuo mkubwa;
- k) Vazi lolote linaloonesha nguo ya ndani;
- l) Nguo yeyote isiyoendana na maadili ya Taifa;

(ii) Nywele zisizofaa:

- a) Nywele chafu;
- b) Nywele ambazo hazikutengenezwa vizuri

3.2.2 Wanafunzi wa Kiume

(i) Mavazi yasiyofaa:

- a) Nguo zinazobana;
- b) Kaptura ya aina yoyote;
- c) Suruali yoyote inayoachwa bila ya kupindwa;
- d) Suruali za '*Jeans*' zinazobana au zilizochanwa;
- e) Kikoi au msuli;
- f) Nguo zenye maandishi ya chama chochote cha siasa na yenye kuonyesha ushabiki wa kitu fulani;
- g) Nguo yeyote inayopingana na maadili ya utumishi wa umma;
- h) Nguo za kubana (Body tight) na kujichora *tattoo*;
- i) Mlegezo;
- j) Vesti aina zote;
- k) '*Jeans*' zenye viraka;

(ii) Nywele zisizofaa:

- a) Nywele chafu
- b) Nywele ambazo hazikutengenezwa vizuri;
- c) Nywele zilizosukwa mtindo wa aina yoyote ile;
- d) Ndevu zisizotunzwa vizuri.

Rejea *Kiambatisho Na. 2* (Kielelezo cha mavazi yasiyofaa kwa wanafunzi wawapo katika mazingira ya Chuo)

3.3 Mavazi na Muonekano Usiofaa kwa Wageni

3.3.1 Wageni wa Kike

(i) Mavazi yasiyofaa:

- a) Nguo zinazobana;
- b) Nguo fupi ambazo zinaacha magoti wazi;

- c) Nguo ambazo zinaacha sehemu ya mwili wazi kama vile kitovu na kifua;
- d) Kaptura aina yoyote ile kama vile pedo na pensi;
- e) Nguo zinazoonyesha maungo ya mwili (*Transparent clothes*);
- f) Suruali za '*Jeans*' zinazobana na kuonesha maungo na zilizochanwa;

3.3.2 Wageni wa Kiume

(i) Mavazi yasiyofaa:

- a) Nguo zinazobana;
- b) Kaptura ya aina yoyote;
- c) Suruali za '*Jeans*' za kubana sana na zilizochanwa;

3.4 Mavazi Yasiyotarajiwa kwa Watumishi, Wanafunzi na Wageni

Kama ilivyoelezwa hapo juu, ni matarajio ya Chuo kuwa kila mtumishi, mwanafunzi au mgeni atazingatia uvaaji unaoendana na mila na desturi za Taifa. Mwongozo huu unaainisha kwa ufupi tu mavazi yasiyotarajiwa kuvaliwa katika mazingira ya Chuo kama vile Nguo ambazo zinaacha sehemu ya mwili wazi kama vile kitovu na kifua, mlegezo, nguo zinazoonyesha maungo ya mwili (*Transparent clothes*), vesti aina zote, jinzi zenye viraka, vazi lolote linaloonyesha nguo ya ndani na kama hizo.

4.0 Utekelezaji wa Mwongozo wa Mavazi Yanayozingatia Maadili kwa Watumishi, Wanafunzi na Wageni

Utekelezaji wa mwongozo huu unahitaji msisitizo na ushirikiano wa makundi yote katika jumuiya ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam. Mwongozo huu ukishaidhinishwa utasambazwa katika ofisi mbalimbali ili kupanua uelewa na uzingativu wa mavazi ya kimaadili Chuoni. Hivyo basi; inapendekezwa hatua zifuatazo kuchukuliwa ili Mwongozo huu uwe na matokeo chanya katika jamii ya Chuo na wageni:

4.1 Kusimika bango kwenye maingilio yote mawili ya Chuo

Chuo kitengeneze na kusimika mabango katika mageti yote mawili ya Chuo yanayoelekeza mavazi yasiyokubalika katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam. Mabango hayo yawe na picha pamoja na maelezo kuhusu mavazi yasiyoruhusiwa ndani ya eneo la Chuo. Mbali na mavazi, mabango husika yafafanue kuhusu viatu, misuko na unyoaji ambao havubaliki katika mazingira ya Chuo.

4.2 Kusambaza mwongozo wa mavazi katika maeneo mbalimbali ya Chuo

Ili kuhamasisha uvaaji wa kimaadili kwa wanajumuiya wa Chuo, mwongozo wa mavazi kwa wanajumuiya ubandikwe katika maeneo mbalimbali ya Chuo, pamoja na kampasi ya Mbagala, ili kuhakikisha kila mwanajumuiya anaufahamu na kuuzingatia.

4.3 Kusambaza Waraka Na. 3 wa Utumishi wa Umma wa Mwaka 2007 kuhusu Mavazi

Kwa kuwa jumuiya ya Chuo inahusisha wanafunzi na wafanyakazi, Chuo kisambaze katika ofisi zote za Chuo waraka Na. 3 wa Utumishi wa Umma wa Mwaka 2007 kuhusu mavazi. Mfanyakazi atakayeshindwa kuuzingatia hataruhusiwa kuingia ndani ya Chuo na atachukuliwa kuwa mtoro ambapo hatua za kinidhamu zitafuata. Waraka husika umeambatanishwa kama *Kiambatisho Na. 3*.

4.4 Kufanya Suala la Kuvaa Mavazi ya Kimaadili Kuwa la Lazima

Kwa kuwa moja ya mambo yanayoonekana kukwamisha jitihada za kuhakikisha kila mmoja anavaa mavazi ya kimaadili Chuoni ni suala hilo kuwa la hiari, Uongozi wa Chuo ufanye suala la mavazi ya kimaadili kuwa la lazima. Ili kuhakikisha hili, Chuo kiwaelekeze walinzi na Polisi Wasaidizi kuhakikisha wanafanya ukaguzi katika maingilio ya Chuo ili kuhakikisha hakuna mtu yeyote aliyevaa kinyume na maadili anaruhusiwa kuingia Chuoni.

4.5 Kusitisha Huduma kwa Muda kwa Watu Wote Ambao Hawajavaa Kimaadili

Uongozi wa Chuo uzielekeze ofisi zote za Chuo kusitisha kwa muda utoaji wa huduma kwa mtu yeyote atakayeingia katika ofisi husika kuhitaji huduma hadi mhusika atakapovaa kimaadili.

4.6 Kuhakikisha Kila Mgeni na Mwanajumuiya wa Chuo Anavaa Kitambulisho

Chuo kihakikishe kuwa kila mwanajumuiya na mgeni wa Chuo anavaa kitambulisho wakati wote anapokuwa katika mazingira ya Chuo. Aidha, Uongozi wa Chuo uagize yeyote ambaye hajavaa kitambulisho asitishiwe huduma mpaka atakapotambulika.

5.0 Hitimisho

Mwongozo huu wa mavazi unategemewa kuleta mabadiliko ya hali ya uvaaji katika jumuiya ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam. Aidha, kila mmoja wetu anapaswa kuuzingatia kuhimizana katika maeneo yetu ya utendaji kazi ili dhamira ya uvaaji unaozingatia mila na desturi ya Taifa ifanikiwe.

Marejeo

Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam. (2018). *Taarifa ya Hali ya Uvaaji na Hatua Zilizochukuliwa na Chuo*. Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam

DUCE. (2015). *Information Guide to Prospective Students*; Dar es Salaam University College of Education.

IFM. (2015). *Kielelezo cha Mavazi Yanayofaa na Yasiyofaa*. Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM). IFM

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (2007). *Waraka wa Utumishi wa Umma Na. 3 wa mwaka 2007 Kuhusu Mavazi kwa Watumishi wa Umma*. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Sheffield Teaching Hospitals. (2010). *Dress Code Policy* [https://www.sheffield.ac.uk/polopoly_fs/1.29489!/file/DressCodePolicy.pdf/](https://www.sheffield.ac.uk/polopoly_fs/1.29489!/file/DressCodePolicy.pdf) ilipakuliwa tarehe 22/3/2018

VIAMBATISHO



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA

**MWONGOZO WA MAVAZI KWA WATUMISHI WA UMMA
KWA MUJIBU WA WARAKA WA UTUMISHI WA UMMA
Na. 3 MWAKA 2007**

BAADHI YA MAVAZI YASIYOFAA KWA WANAUUME



- Nguo ambazo ni za kazi maalum kama vile michezo (Hizi zivaliwe wakati wa shughuli hiyo tu.)
- Nguo ambazo zina michoro, maandishi na picha ambazo hazierendani na shughuli za serikali.
- Nguo zinazobana.
- Kaptura ya aina yoyote.
- Suruali yoyote inayoachwa bila kupindwa.
- Suruali za "Jeans" na Fulana "T-shirts" (Hizi zivaliwe tu wakati wa shughuli maalum inayotambulika)
- Kikoi au msuli.
- Nguo zenye maandishi ya chama chochote cha siasa na yenye kuonyesha ushabiki wa kitu fulani.
- Nguo yoyote inayopingana na maadili ya utumishi wa umma.

BAADHI YA MAVAZI YASIYOFAA KWA WANAWAKE




- Nguo zinazobana.
- Nguo fupi ambazo zinaacha magoti wazi.
- Nguo ambazo zinaacha sehemu ya mwili wazi kama vile kitovu na kifua.
- Nguo ambazo zina picha, michoro, na maandishi ambayo hayaendani na shughuli za serikali.
- Kaptura aina yoyote ile kama vile pedo na pensi.
- Nguo zinazoonyesha maungo ya mwili (transparent).
- Suruali za 'Jeans'
- Suruali yoyote iliyoachwa bila kupindwa.
- Fulana - 'T-Shirts' (Hizi zivaliwe tu wakati wa shughuli maalumu inayotambulika.)

CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA ELIMU DAR ES SALAAM

MWONGOZO WA MAVAZI KWA WANAFUNZI

BAADHI YA MAVAZI YASIOFAA KWA WANAFUNZI WAWAPO KATIKA MAZINGIRA YA CHUO



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

Anwani ya Simu: "UTUMISHI" DSM
Utumishi wa Umma,
Simu: 2118531/4
Fax: 2125299/2127806
Dar es Salaam.
Barua Pepe: permsec@estabs.go.tz



Menejimenti ya

P. O. Box 2483,

TANZANIA.

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. EG.45/86/01/"A"/2

12/9/2007

**WARAKA WA UTUMISHI WA UMMA NA 3 WA MWAKA 2007
KUHUSU MAVAZI KWA WATUMISHI WA UMMA**

Utangulizi:

Waraka wa Utumishi Na. 1 wa mwaka 1971 unaohusu mavazi ulitokana na mwongozo uliotolewa na Chama cha TANU kuhusu mavazi.

Madhumuni ya waraka huo ilikuwa kuimarisha heshima ya Taifa kwa kuhakikisha kuwa watumishi wa Serikali wanavaa mavazi ya heshima wanapowahudumia wananchi. Waraka huo uliainisha baadhi ya mifano ya mavazi ambayo yalionekana hayafai na yale yanayofaa kwa wanawake na wanaume, utengenezaji wa nywele unaofaa na usiofaa na vipodozi visivyokubalika.

Hali ilivyo sasa:

2. Tangu waraka huo ulipotolewa kumekuwepo na mabadiliko makubwa ya mitindo ya mavazi, nywele na vipodozi. Mabadiliko ya mitindo ya mavazi ni jambo lisiloepukika. Hata hivyo baadhi ya mitindo hiyo ya mavazi inashusha heshima na hadhi ya utumishi wa umma kama itaendelea kuvaliwa na ni kinyume na kifungu cha 2 (e) cha kanuni za Maadili ya utendaji katika utumishi wa umma za mwaka 2005. Hata hivyo kumekuwepo na tatizo la kutokuwepo na tafsiri inayoeleweka juu ya mavazi gani ni ya heshima au yanayokubalika na yasiyokubalika mahali pa kazi.

Uamuzi wa Serikali:

Tafsiri ya mavazi ya heshima hutegemea mila na desturi ya jamii husika. Katika utumishi wa umma mavazi ya heshima kwa mtumishi wa umma ni yale ambayo yanazingatia mila na desturi za taifa letu ambayo yanapovalika hayaonyeshi sehemu ya maungo ya mwili ambayo hayakuzoeleka kuachwa wazi, hayabani na ambayo hayana michoro au maandishi ya kudhalilisha wengine au yanayoonyesha ushabiki wa kitu fulani.

Kwa hiyo waraka huu unatoa ufafanuzi kuhusu mavazi nadhifu yanayopaswa kuvaliwa kazini kwa kutoa mifano michache ya mavazi ambayo siyo ya heshima na ambayo hayakubaliki katika utumishi wa umma kwa jinsi zote mbili.

Utekelezaji:

Ufuatao ni ufafanuzi wa mavazi yasiyokubalika mahali pa kazi ambayo pia yameonyeshwa kwa picha kwenye kiambatisho A na B. Nguo kama “Jeans” na fulana zinaweza kuvaliwa na watumishi ambao wanalazimika kufanya kazi za nje ya ofisi.

Kwa Wanawake

(i) Baadhi ya mavazi yasiyofaa:

Nguo zinazobana,

Nguo fupi ambazo zinaacha magoti wazi.

Nguo ambazo zinaacha sehemu ya mwili wazi kama vile kitovu na kifua,

Nguo ambazo zina picha, michoro, na maandishi ambayo hayaendani na shughuli za serikali,

Kaptura aina yoyote ile kama vile pedo na pensi, • Nguo zinazoonyesha maungo ya mwili (transparent).

Suruali za “Jeans”,

Suruali yoyote iliyoachwa bila kupindwa,

Fulana – “T-Shirts” (Hizi zivaliwe tu wakati wa shughuli maalum inayotambulika),

Nguo ambazo ni za kazi maalum – michezo, kazi za nje au burudani. Hizi zivaliwe mahususi wakati wa utekelezaji wa shughuli hizo, Nguo yenye maandishi ya chama chochote cha siasa au ushabiki wa kitu fulani,

Nguo yeyote inayopingana na maadili ya utumishi wa umma.

(ii) Nywele zisizofaa:

• Nywele chafu na ambazo hazikutengenezwa vizuri.

Viatu visivyofaa

Kandambili,

Viatu vya michezo (isipokuwa wakati wa shughuli maalum za michezo),

Kwa Wanaume

(i) Baadhi ya mavazi yasiyofaa:

Nguo ambazo ni za kazi maalum kama vile michezo (Hizi zivaliwe wakati wa shughuli hiyo tu),

Nguo ambazo zina michoro, maandishi na picha ambazo haziendani na shughuli za serikali.

Nguo zinazobana,

Kaptura ya aina yoyote,

Suruali yoyote inayoachwa bila kupindwa,

Suruali za “Jeans” na Fulana “T-shirts” (Hizi zivaliwe tu wakati wa shughuli maalum inayotambulika),

Kikoi au msuli,

Nguo zenye maandishi ya chama chochote cha siasa na yenye kuonyesha ushabiki wa kitu fulani.

Nguo yeyote inayopingana na maadili ya utumishi wa umma.

(iii) Nywele zisizofaa:

Nywele chafu na ambazo hazikutengenezwa vizuri. • Nywele zilizosukwa mitindo ya aina yoyote ile

Ndevu zisizotunzwa vizuri.

Viatu visivyofaa:

Kandambili,

Viatu vya michezo(Labda wakati wa shughuli maalum za michezo).

Mwisho:

Kwa waraka huu waajiri wote wanapaswa kuwaelimisha watumishi kuhusu mavazi yasiyokubalika na kusimamia kikamilifu suala la mavazi kwa watumishi wa umma .

Waraka huu unafuta Waraka wa Utumishi Na.1 wa mwaka 1971 na unaanza kutumika mara moja.

George D. Yambesi

KATIBU MKUU

(MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA)